



TAARIFA KWA UMMA

NJIA MPYA ZA USAJILI WA LESENI MKOANI DODOMA

Dodoma,

26 Juni, 2024.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawakaribisha wasafirishaji kuomba leseni kwenye njia mpya za Daladala Jijini Dodoma, kwa lengo la kufikisha huduma karibu na wananchi kwa mabasi yanayokidhi vigezo kama ifuatavyo;

| NA | KUTOKA | KWENDA | KUPITIA | UJAZO WA BASI KUENZIA ABIRIA | IDADI |
|----|------------------|-----------|-----------------|------------------------------|-------|
| 1 | MACHINGA COMPLEX | CHIDACHI | KIKUYU | 25 | 20 |
| 2 | MACHINGA COMPLEX | ST. GEMA | MPAMAA | 25 | 20 |
| 3 | MACHINGA COMPLEX | ILAZO | MELIWA | 25 | 20 |
| 4 | MACHINGA COMPLEX | NJEDENGWA | KISASA | 25 | 20 |
| 5 | MACHINGA COMPLEX | VIKONJE | MJI WA SERIKALI | 25 | 20 |

Vigezo vya kuzingatia:

1. Kwa gari jipya ambalo halijawahi kusajiliwa katika mfumo wa utoaji leseni wa RRIMS, Mtoa huduma hakikisha unafika Ofisi ya LATRA Mkoa wa Dodoma kupatiwa namba ya utambulisho.
2. Hakikisha gari imekaguliwa na Jeshi la Polisi na kupata hati ya ukaguzi.
3. Fanya maombi ya leseni kupitia mfumo wa RRIMS kwa kiunganishi www.rrims.latra.go.tz

Imetolewa na:
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano